



SHIYANGA REGION CO – PERATIVE UNION (1984) LTD

P. O. BOX 349, SHINYANGA, TEL/FAX 255 28 2762525

Email:info@shireculimited.co.tz Website:www.shireculimited.co.tz

KUMB. NA.SRCU/TB/39/VOL.II/53

TAREHE : 11/04/2025

A. TANGAZO LA ZABUNI

1. Chama kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga ni Chama kilichosajiliwa kwa **Na.AFF-SHY-SHY-MC-2022-9** na hufanya kazi chini ya sheria ya Vyama vya Ushirika Namba **6** ya mwaka **2013** pamoja na kanuni zake za mwaka **2015**. Maeneo ya shughuli za Chama hiki ni Mkoa wa Shinyanga katika Wilaya ya Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini na Kishapu.
2. Kwa idhini ya Bodi ya chama Kikuu, Mwenyekiti wa bodi anatangaza zabuni shindanishi ya Kitaifa (National Competitive Tendering) kwa zabuni ya **UNYUNYIZAJI DAWA (FUMIGATION) MAGHALA .**

B. MAHITAJI YA ZABUNI

| ZABUNI NA. | MAELEZO YA ZABUNI |
|----------------------------------|---|
| SRCU/2025-2026/ZBN/FMG/01 | Zabuni ya unyunyizaji Dawa (fumigation) Maghala kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 |

Chama kinatangaza : **ZABUNI YA UNYUNYIZAJI DAWA (FUMIGATION) katika maghala yaliyopo katika Kanda ya KISHAPU, Kanda ya UZOGOLE, na Kanda ya SOLWA**

3. Mchakato wa zabuni hii utafanyika kwa njia shindanishi ya kitaifa (National Competitive Tendering) kwa mujibu wa Mwongozo wa Ununuzi na Ugavi wa vyama vya Ushirika Tanzania Bara, Sheria na Kanuni za manunuzi ya umma na ni zabuni ya wazi kwa wazabuni wote wenye sifa zinazohitajika.
4. Kitabu cha zabuni kitapatikana baada ya kulipia ada ya Zabuni kwa gharama ya Fedha za Kitanzania Shilingi Laki TANO tu (500,000) ambazo hazitarudishwa. Fedha zote zilipwe kwenye nambari ya akaunti **01J1058431301** jina la Akaunti **SHIRECU (1984) LTD Benki ya CRDB**. Ukishalipa njoo na uthibitisho wa malipo (Bank slip)
5. Waombaji wawasilishe zabuni zao (Nakala mbili) nakala halisi moja na kopi moja zikiwa zimefungwa kwenye bahasha kwa umakini na kutiwa lakiri.
6. Muda wa kutuma maombi ya Zabuni ni siku saba 7 baada ya Tangazo kutolewa kuanzia tarehe 11 .April. 2025 hadi tarehe 17 April, 2025 saa Nne kamili asubuhi na SIKU HIYO NDIO SIKU YA UFUNGUZI.
7. Zabuni zitakazochelewa hazitapokelewa wala kufanyiwa kazi wakati wa tathimini ya Zabuni bila kujali sababu zozote za kuchelewa kwazo.

C. SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Mmiliki wa Kampuni iliyosajiliwa na **BRELA** na yenye namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi [**TIN**]
- ii. Kampuni iwe na uwezo na uzoefu wa kuendesha shughuli za Fumigation
- iii. Kampuni iwe na watumishi wenye uwezo na sifa kutoka TRPI / TPHA
- iv. Kampuni iwe na vitendea kazi VIZURI vya kutosha vya kufanya kazi iyo
- v. Kampuni iwe na Leseni hai ya kuendesha Shughuli za Fumigation
- vi. Kampuni iwe haijawahi kusababisha hasara katika kazi zake.
- vii. Waombaji wawe na kitambulisho cha NIDA.

MAOMBI YOTE YAANDIKWE KWA KUZINGATIA YAFUATAYO:

Tarehe ya mwisho kuwasilisha maombi ni siku ya **Alhamisi, April 17, 2025 saa 4:00 asubuhi (Saa nne kamili asubuhi)** na **SIKU HIYO ITAKUWA NI SIKU YA UFUNGZI** utakaofanyika Makao makuu ya Ofisi ya Chama kikuu cha Ushirika [**SHIRECU (1984) LTD**], Waombaji wote mnashauriwa kuhudhuria wenyewe bila kutuma wawakilishi.

Maombi ya Zabuni yatakayowasilishwa Ofisi ya Chama kikuu [**SHIRECU (1984) LTD**] yafungwe ndani ya bahasha kwa **LAKIRI** au kutumwa kwa barua pepe info@shireculimited.co.tz yakiwa katika faili moja aina ya PDF.

Barua iandikwe kwa;

**KAIMU MENEJA MKUU,
SHIRECU (1984) LTD,
S. L. P. 349,
SHINYANGA.**

Kwa maelekezo zaidi kuhusiana na Zabuni hii tafadhali usisite kuwasiliana nasi kwa kupitia simu namba 0755 556 228 au barua pepe info@shireculimited.co.tz

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA :

.....
LENIS JISHANGA IZENGO

MWENYEKITI WA UONGOZI WA BODI

SHINYANGA CO – OPERATIVE UNION (1984) LTD

